# TAARIFA KWA WAPIGA KURA WALIOKO PENNSYLVANIA



Kuna uchaguzi
JUMANNE,
**NOVEMBA 5.**

## JUA HAKI ZAKO

# UNA HAKI!

**Unaweza kujisajili na kupiga kura ikiwa:**

- Wewe ni raia wa Marekani
- Una umri wa miaka 18 au zaidi ifikapo Siku ya Uchaguzi
- Wewe ni mkaazi wa Pennsylvania

**Kila mtu anayestahiki ana haki ya kupiga kura.**
Ili kupata maelezo yaliyosasishwa kuhusu uchaguzi, kupata usaidizi kuhusu suala lolote linalohusiana na kupiga kura, au kuripoti tatizo katika Siku ya Uchaguzi, unaweza kupiga simu kwa mojawapo ya namba hizi za dharura zisizopendelea chama chochote:

Kiingereza: **866-OUR-VOTE (866-687-8683)**
Kamati ya Mawakili ya Haki za Kiraia Chini ya Sheria

Kihispania na Kiingereza: **888-VE-Y-VOTA (888-839-8682)**
Mfuko wa Elimu wa NALEO

Kiarabu na Kiingereza: **844-YALLA-US (844-925-5287)** عربى)
Taasisi ya Kiarabu ya Marekani (AAI)

Kimandarini, Kikantoni, Kikorea, Kivietinamu, Kitagalogi, Kiurdu, Kihindi, Kibengali na Kiingereza - **888-API-VOTE (888-274-8683)**
APIAVote & Asian Americans Advancing Justice (AAJC)

Simu ya video ya lugha ya ishara ya Marekani: **301-818-VOTE (8683)** Chama cha Kitaifa cha Viziwi (NAD)

Unaweza pia kupigia simu ofisi ya uchaguzi ya jimbo ili upate usaidizi, ikiwa ni pamoja na jinsi ya kupata ofisi ya uchaguzi ya jiji au kaunti yako: **1-877-VOTESPA**

# UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

## Kujisajili kupiga kura

**Nilijisajili kupiga kura hivi majuzi. Je, nitahakikisha vipi kuwa nimesajiliwa?** Ilnachukua siku chache ili ofisi ya uchaguzi ya kaunti ipitie fomu yako ya usajili na iandike jina lako kwenye orodha.

- Unaweza kuangalia hali yako ya usajili kwa kupigia simu bodi ya uchaguzi ya kaunti yako au kwenda mtandaoni kwa **www.pavoterservices.pa.gov/Pages/voterregistrationstatus.aspx**
- Ukipata arifa kwamba usajili wako umekataliwa, au ukiwa na swali, pigia simu **866-OUR-VOTE** ili upate usaidizi.

## Mimi ni mpiga kura aliyesajiliwa, lakini nilihama hivi majuzi. Je, bado nimejisajili kupiga kura?

- Ndiyo. Ila, ikiwa ungependa kupiga kura karibu na nyumba yako mpya, au ikiwa unataka kupiga kura kwa njia ya barua ya posta, utahitaji kusasisha usajili wako kwa kuandika anwani yako mpya. Unaweza kubadilisha anwani yako mtandaoni katika Idara ya Jimbo ya PA. Ikiwa unataka kujisajili ana kwa ana, au kwa karatasi, piga simu namba ni **1-877-VOTESPA** ili upate usaidizi.
- Unaweza pia kurudi kwenye kituo chako cha zamani cha kupigia kura na upige kura huko. Iwapo ulihama chini ya siku 30 kabla ya uchaguzi, ni lazima upige kura katika kituo chako cha zamani cha kupigia kura. Ikiwa ulihama kutoka nje ya jimbo, unahitaji kujisajili kupiga kura hapo Pennsylvania.

## Je, ninaweza kujisajili na kupiga kura ikiwa nimeshtakiwa kwa kuhusika katika uhalifu?

- Ndiyo, unaweza kupiga kura mradi haujafungwa kwa kosa la jinai kwa sasa. Unaweza kupiga kura ikiwa uko katika kipindi cha majaribio au kifungo cha nje, ukiwa chini ya kifungo cha nyumbani, au ikiwa unatumikia kifungo kwa ajili ya kosa dogo.

## Nilizaliwa Puerto Rico. Je, ninaweza kupiga kura katika jimbo la Pennsylvania?

- Ikiwa ulizaliwa Puerto Rico, wewe ni raia wa Marekani kiotomatiki na unaweza kujisajili kupiga kura katika jimbo la Pennsylvania (au jimbo unaloishi).

***Kupiga kura au hata kujisajili kupiga kura wakati wewe si raia wa Marekani ni uhalifu na kunaweza kukuzuia kuwa raia.***

# KUPIGA KURA KWA BARUA YA POSTA

## Je, ninatuma vipi ombi la kura ya barua ya posta?

- Tuma ombi la kura ya barua au ya kutohudhuria kituo cha kupigia kura kwa **votesPA.com**.

## Je, nifanye nini ikiwa ombi langu la kura ya barua ya posta limekataliwa?

- Ukipata notisi kwamba ombi lako lilikataliwa, piga simu kwa **866-OUR-VOTE** ili usaidiwe bure na wakili.

## Nitapata kura yangu lini?

- Kwa mujibu wa sheria, lazima kaunti ikutumie kura yako ya barua ya posta wiki mbili kabla ya uchaguzi. Iwapo haitafika, au ukiipoteza, au ukifanya makosa unapotia alama kwenye kura, pigia simu ofisi yako ya uchaguzi ya kaunti ili wakupe nyingine.
- Unaweza kuangalia au kufuatilia kura yako kwenye **https://vote.pa.gov/mailballotstatus**

## Je, mtu mwingine anaweza kunipelekea kura yangu ya barua ya posta?

- Lazima urudishe kura yako mwenyewe. Ikiwa una ulemavu unaweza kuteua mtu mwingine akurudishie kura yako kwa kujaza fomu ya Wakala Aliyeidhinishwa katika **www.VotesPA.com**.

## Je, ninaweza kubadilisha mawazo yangu kuhusu kupiga kura kwa barua ya posta baada ya kutuma ombi?

- Ndiyo. Lete kura yako na bahasha ya kurejesha katika kituo chako cha kupigia kura Siku ya Uchaguzi. Wafanyikazi wa kura wataighairi, na unaweza kupiga kura ana kwa ana katika kituo cha kupigia kura. Ikiwa huna kura yako, itabidi upige kura ya muda.

## Je, kura yangu itahesabiwa kweli nikipiga kura kwa barua ya posta?

- Kupiga kura kwa barua ya posta ni salama. Kuna ukaguzi unaofanya ili kuhakikisha kuwa kura yako inahesabiwa. Ikiwa unashuku kuwa kura imepotea katika barua ya posta, au ukiipoteza nyumbani, unaweza kupigia simu ofisi yako ya uchaguzi ya kaunti na kuomba nyingine. Tafuta ofisi ya uchaguzi ya kaunti yako kwenye Google, au upige simu kwa **1-877-VOTESPA** ili uunganishwe

## Ili kura yako ihesabiwe lazima:

- Uingize kura yako iliyotiwa alama kwenye bahasha ya siri, iliyoandikwa "Kura Rasmi ya Uchaguzi." Funga bahasha na usiandike chochote kwenye bahasha hiyo
- Uingize bahasha ya siri iliyofungwa kwenye bahasha ya nje ya kurejesha yenye anwani ya kaunti
- LAZIMA utie sahihi kwa kuandika jina lako na tarehe kwa mkono kwenye bahasha ya kurejesha.
- Usipotia sahihi na kuandika tarehe kwenye bahasha kura yako HAITAHESABIWA.

# KUPIGA KURA ANA KWA ANA

## Ninapaswa kupiga kura wapi?

Unaweza kupata kituo chako cha kupigia kura kwenye **www.votesPA.com**, kwa kupiga simu kwa **866-OUR-VOTE** au kwa kupigia simu afisi yako ya uchaguzi ya kaunti.

## Je, ninahitaji kitambulisho cha picha ili nipige kura ana kwa ana?

Hapana. Wapiga kura wanaopiga kura kwa mara ya kwanza katika kituo chao cha kupigia kura pekee ndio wanahitaji kuonyesha kitambulisho. Unaweza kutumia kitambulisho cha picha, ikiwa ni pamoja na kitambulisho cha mfanyakazi au mwanafunzi ikiwa unayo. Unaweza pia kutumia kitambulisho kisicho cha picha, kama vile bili ya huduma au taarifa ya benki iliyo na anwani yako. Hupaswi kuombwa kitambulisho chako ikiwa ulipiga kura hapo awali katika kituo hicho cha kupigia kura.

## Je, wakiniambia kuwa jina langu halipo kwenye orodha ya wapiga kura?

Kwanza, mwombe afisa wa uchaguzi aangalie orodha tena au aangalie kitabu cha ziada cha kura (orodha ya mabadiliko ya hivi majuzi kwenye orodha za wapiga kura). Jitolee kutamka jina lako. Ikiwa unaamini kuwa uko katika kituo sahihi cha kupigia kura lakini jina lako haliko kwenye orodha ya wapiga kura, omba kura ya muda, wanatakiwa kukupa. Tafadhali ripoti mambo uliyopitia kwa **866-OUR-VOTE.**

## Je, kura ya muda ni nini?

Kura ya muda hutumika kurekodi kura yako wakati kuna swali kuhusu ustahiki wako au ikiwa uliomba kura ya barua ya posta. Itahesabiwa iwapo maafisa wa uchaguzi watabaini kuwa ulistahiki kupiga kura.

## Je, haki yangu ya kupiga kura inaweza kupingwa katika kituo cha kupigia kura?

Ndiyo, lakini kwa sababu fulani na watu fulani. Afisa wa uchaguzi, mwangalizi wa shughuli za kupiga kura, au mpiga kura mwingine anaweza tu kumpinga mpiga kura ikiwa anafikiri kuwa mpiga kura huyo haishi katika jimbo la uchaguzi au ni mtu anayejifanya mtu mwingine.

# TAREHE KUU ZA UCHAGUZI MKUU



- Jisajili ili upige kura tarehe **21 Oktoba.**
- Tuma omba la kura ya barua ya posta tarehe **29 Oktoba.** Inapendekezwa kuwa uwasilishe ombi kabla ya tarehe 21 Oktoba.
- Rudisha kura ya barua ya posta kabla ya saa **8 p.m. tarehe 5 Novemba.** Inapendekezwa kuwa uirudishe kabla ya tarehe 30 Oktoba.

Kwa taarifa zaidi, tembelea **www.votesPA.com**

**Kanusho**
Mwongozo huu wa kupiga kura katika jimbo la Pennsylvania sio ushauri wa kisheria. Ikiwa una maswali kuhusu kustahiki au haki zako, tafadhali piga simu kwa **866-OUR-VOTE** au wasiliana na wakili.